Nia Dhidi Ya Kanisa

Au Mnalidharau?

(Attitude Towards The Church — Do You Despise It?)

Na

Ellis P. Forsman

Nia Dhidi Ya Kanisa
Au Mnalidharau?
(Attitude Towards The Church — Do You Despise It?)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Nia Dhidi Ya Kanisa
Au Mnalidharau?
1 Kor. 11:22

Kidini tunaweza kuwa na nia inayoleta Baraka kutoka kwa Mungu, au ambayo haileti Baraka. Tulijifunza nia zetu dhidi ya Mungu, Yesu Kristo, na injili; sasa tutajifunza kuhusu nia zetu dhidi ya kanisa.

Nia ambayo mtu huonyesha dhidi ya kanisa ni jambo ambalo linaumuhimu mkubwa.

1 Kor. 11:22, "*Je! Hamna nyumba za kulia na kunywea? Au mnalidharau kanisa lake Mungu? Na kuwatahayarisha hao wasio na kitu? Niwaambieni? Niwasifu? La! Siwasifu kwa ajili ya hayo.*"

Moja kati ya maswali yanayotushitaki ambalo halijawahi kuulizwa na Mtume Paulo ni moja lililoko katika kifungu chetu, na linahusu nia yetu dhidi ya kanisa.

Kimsingi swali ambalo Paulo aliuliza kimsingi lilikuwa na muunganiko na Wakorintho waliokuwa wakichafua meza ya Bwana.

Paulo aliona kuwa walikuwa wakiipotosha kwa kuifanya kuwa chakula cha kawaida ambapo kila mmoja alileta chakula chake kutoka nyumbani, na kwa sababu hiyo Paulo akaandika ili kupinga. 1 Kor. 11:17, "*Lakini katika kuagiza haya siwasifu ya kwamba mnakusanyika, si kwa faida bali kwa hasara.*"

Swali hili, "*Au mnalidharau kanisa lake Mungu?*" linaenda zaidi ya meza ya Bwana; linaweza pia kuhusishwa na uhusiano wetu na kanisa.

"Dharau" – kuweka chini; kutokuthaminisha; kutokujali; kuharibu; kupotosha; kukataa."

Kanisa linaweza kutazamwaje kwa mtazamo ya chini, kutothaminishwa, kutojaliwa, kuharibiwa, potoshwa , na kukataliwa?

Tunaweza kulidharau kanisa kwa kumkataa Kristo kuwa kichwa chake

- 1 Kor. 12:27, "*Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila mmoja pekee yake.*"
- Efe. 5:30, "*Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake.*"

Katika muunganiko huu tunaona ushirika wa kanisa na mfumo mkuu wa Agano Jipya. Sawa na jinsi kulivyo na ukimwa katika mwili wa damu na nyama, ndivyo kunapaswa kuwa na umoja katika mwili wa Kristo, ambalo ndiyo kanisa lake.

Rum. 12:4-5, "*Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja; vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo kila mmoja kwa mwenzake.*"

Lakini kwa nini kuna hisitoria katika mwili wa damu na nyama? Kwa sababu kila kiungo cha mwili kinatii kichwa na ni kichwa kimoja tu.

Ikiwa wale wanao tabiri kuwa ni viungo vya mwili wa Kristo wangemtambua Kristo kuwa ndiye kichwa, kusingekuwa na vitu kama madhahebu, mifumo, na migawanyiko.

Kristo hakufanywa kichwa cha kanisa hadi wakati alipofufuka kutoka katika wafu. Kabla ya kifo chake alidai kwamba hasingeweza kufanya cho chote. Yoh. 5:19, "*…Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile.*"

Lakini baada ya kufufuka kwake akasema, Mathayo 28:18, "*…Mamlaka yote nimepewa mimi mbinguni na duniani.*"

Lakini Kristo alifufuliwa kutoka katika wafu ili asife tena. Rum. 6:9, "*Tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu, hafi tena wala mauti haimtawali tena.*"

Alishinda kifo nab ado anaishi miongoni mwetu, lakini ni katika Roho, si katika mwili. Hivyo, Kristo hatakufa tena na kuacha sehemu yake akiwa kama kichwa cha kanisa kwa mwili wa damu na nyama. Bado ana uwezo huo na mamlaka ambayo Mungu amempa.

Yesu bado ataendelea kuwa kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa hadi atakaporudi kwa mara ya pili. Efe. 1:22, "*Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa.*"

Bado anatoa mwongozo kwa kanisa. 1 Kor. 15:24, "*Hapo ndipo mwisho atakapompa Mungu Baba ufalme wake, atakapobatilisha utawala wote na mamlaka, na nguvu.*"

Hii itatokea katika kurudi kwake mara ya pili.

Hivyo basi, hatupaswi kuangalia mwili wa damu na nyama duniani kama kichwa cha mwili, na kitengo cho chote ambacho mwanamume au mwanamke ndiyo kichwa haiwezi kuwa kanisa lake Kristo, kwa sababu Kristo bado angali kichwa cha kanisa.

Tunaweza kulidharau kanisa kwa kutokuwa na maudhurio ya ibada zake

Kila Mkristo anapaswa kufanya jitihada katika kuhudhuria kanisani. Tunapaswa kwendana na swala la dhamira, nafasi, na wajibu.

Tunapaswa kuwa katika huduma ya Bwana kwa sababu hilo ni agizo la Bwana. Ebr. 10:25-26, "*Wala tusiache kukusanyika pamoja kama ilivyo desturi yaw engine, bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia. Maana kama tukifanya dhambia kusudi baada ya kuupokea ile kweli haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi.*"

Kila wakati tunakusanyika pamoja katika huduma ya ibada, kila mkristo anapaswa kufurahi kuwepo pale.

Tunapaswa kuwa na nia kama ambayo Daudi alikuwa nayo kuhusiana na kusanyiko. Zab. 122:1, "*Nalifurahi waliponiambia, na twende nyumbani kwa BWANA.*"

Tunaona katika maneno haya msukumo ambao Daudi alichukua katika kuufikia nyumba ya Bwana na kuingia ndani kumwabudu Mungu. Daudi alifurahi alipopata nafasi hii.

- Zab. 84:1-4, "*Maskani zako zapendeza kama nini, ee BWANA wa majeshi. Nafsi yangu imezionea shauku nyua za BWANA. Naam, na kuzikondea. Moyo wangu na mwili wangu vinamlilia Mungu aliye hai. Shomoro naye ameona nyumba , na mbayuwayu amejipatia kioto, alipoweka makinda yake, kwenye madhabahu zako, ee BWANA wa majeshi, mfalme wangu na Mungu wangu. Heri wakaao nyumbani mwako, wanakuhimidi daima.*"

- Zab. 84:10, "*Hakika siku moja katika nyua zako ni bora kuliko siku elfu. Ningependa kuwa bawabu nyumbani mwa Mungu wangu kuliko kukaa katika hema za uovu.*"

Nia kuu ambayo Daudi alikuwa nayo dhidi ya kusanyiko!

Yoh. 4:24, "*Mungu ni Roho <u>nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika roho</u> na kweli.*" Tunapaswa kumwabudu Mungu kulingana na mfumo aliotupatia, na pia tupaswa kumwabudu katika roho na furaha.

Wakristo wa kwanza walimwabudu Bwana kila mara. Mdo. 2:42, "*Wakawa <u>wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika</u>, na katika kuumega makate, na katika kusali.*"

Walikuwa wakidumu katika kusanyiko. Hawakuruhusu cho chote kiwaingilie kati.

Mdo. 11:26, "*Hata alipokwisha kumwona akamleta mpaka Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia.*"

Ndiyo, kanisa la kwanza lili simama imara katika kusanyiko lao. Mara ngapi? Mdo. 20:7, "*Hata siku ya kwanza ya juma tulipokuwa tumekutana ili kuumega mkate, Paulo akawahutubu akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane.*"

Sehemu za kazi za watu wengine siku ya malipo ni Ijumaa. Wanatarajia kulipwa kila ijumaa. 1 Kor. 16:1-2, "*Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia nanyi fanyeni hivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ilikwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja;*"

Ndugu na dada zangu, neno la Mungu **linatuambia** kuwa kusanyiko lilikuwa kila Juma pili. "*Kila siku ya kwanza ya juma.*" – kata mian sabatoon" – "kila siku ya kwanza ya juma."

Tunaweza kulidharau kanisa kwa kushindwa kufanya maandalizi kwa ajili ya ibada

Mungu anapaswa kuabudiwa "*katika roho na kweli*" (Yohana 4:24). Ye yote anayehubiri anapaswa kuuandaa ujumbe wake. Anapaswa kujifunza, fikiri, kusoma, na kuomba kuhusu somo lo lote ambalo ameandaa kwa ajili ya kuonya, kuinua, na kuwatia moyo watu wa Mungu.

Pia, kusanyiko nalo linapaswa kujiandaa kwa ajili ya ibada katika nyumba ya Bwana. Wanaume wanapaswa kujiandaa kwa kila kitu watakaoambiwa kulifanya: Kuongoza nyimbo, sala, Meza ya Bwana, nk.

Lakini wote tunapaswa kuandaa mioyo yetu kwa ajili ya ibada.

Kwa upande wa meza ya Bwana, Yesu alisema: Marko 4:24, "*…Angalieni msikialo, kipimo kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa, na tena mtazidishiwa.*"

Sikiliza kile kinacho fundishwa. Likague. Msiwe kama makanisa ya dunia ambapo yanayofundishwa hayakaguliwi.

Pia akasema katika Luka 8:18, "*Jiangalieni basi jinsi msikiavyo, kwa kuwa mwenye kitu atapewa, na yule asiye na kitu atanyang'anywa hata kile ambacho anadhaniwa kuwa anacho.*"

Je akili yako iko katika kitu ambacho unafikiria kufanya baada ya ibada kuisha? Je unafikiria kuhusu mpira ulioangalia jumamosi? Je

unasikiliza neno la Mungu kidogo likihubiriwa kwa sababu kuna kitu kinakusumbua akilini. "*Jiangalieni basi jinsi msikiavyo…*"

Katika kusanyiko la watakatifu ambapo kunapaswa kuwe na ibada na heshima, kwa sababu Bwana wetu amesema yu katikati yetu tunapokusanyika kwa ajili ya jina lake.

- Mat. 18:20, "*Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.*"
- Yoh. 12:26, "*…Nilipo mimi ndipo mtumishi wangu atakapokuwepo…*"
- Zab. 89:7, "*Mungu huogopwa sana barazani pa watakatifu, ni wa kuhofiwa kuliko wote wanaomzunguka.*"

Huu ni wakati wa kumtazama Mungu.

Kusanyiko la kanisa letu linapaswa kuwa katika hali ya ukimya, kama jinsi ilivyokuwa kwa wana wa Israeli. Nimewahi kuwa katika makusanyiko ambalo kila mtu alikuwa anaongea na kiongozi ilibidi apige kelele ili wawe kimya; na pia nimewahi kuwa katika makusanyiko mengine ambapo kila mmoja alikuwa amekaa na kimya kwa utayari wa dakika chache kabla ya.

Mungu aliwaambia wana wa Israeli: Kut. 20:8, "*Ikumbuke siku ya sabato uitakase.*"

Tunapaswa pia kuitunza kusanyiko la Bwana takatifu, kwa sababu yu pamoja nasi.

Tunaweza kulidharau kanisa katika dini zetu za raha imani na vishawishi

Tunapaswa kukifahamu kile tunacho kiamini na kwa nini tunakiamini.

1 Pet. 3:15, "*Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na hofu.*"

Fahamu kile tunachokiamini katika ukuu wa Yesu, katika uzao wake wa bikra, Ubwana wake, ufalme wake, kifo chake na ufufuo.

Jua kwamba wokovu ni kupitia Yesu na kanisa lake.

- Yoh. 14:6, "*Yesu akamwambia mimi ndimi njia kweli na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"
- Mdo. 2:47, "*Wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote, Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*"

Jua kwamba neno lake linapaswa kuwekwa safi.

- Mdo. 4:20, "*Maana sisi hatuwezi kuacha mambo tuliyoyaona na kuyasikia.*"
- Ufu. 22:18-19, "*Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.*"

Hiyo inatia maanani, siyo!

Tunaweza kulidharau kanisa kwa dunia na maisha yetu yasiyofaa ambayo hayaendani na ujuzi wetu

Wakristo wanapaswa kushikilia viwango vyote na dhumuni la tabia katika maisha yao ya kila siku kama inavyofundishwa katika neno la Mungu.

Rum. 2:21-24, "*Basi wewe umfundishaye mwingine, je! Hujifunzi mwenyewe? Wewe uhubiriye kwamba mtu asiibe, waiba mwenyewe? Wewe usemaye kwamba mtu asizini, wazini mwenyewe? Wewe uchukiaye sanamu, wateka mahekalu? Wewe ujisifuye katika torati, wamvunjia Mungu heshima kwa kuiasi torati? Kwa maana jina la Mungu latukuzwa katika mataifa kwa ajili yenu, kama ilivyoandikwa.*"

Maisha yetu katika juma nzima lazima yawe matakatifu. 1 Kor. 10:31-32, "*Basi mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu. Msiwakoseshe Wayahudi wala Wayunani wala kanisa la Mungu.*"

Kama Wakristo wakifanya mambo haya katika maisha yao ya kila siku, basi ni wafuassi wa kweli wa Kristo.

Mat. 5:13-16, "*Ninyi ni chumvi ya dunia lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu. Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu yam lima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.*"

Je wengine wanakwambia kuwa lazima ufanyike Mkristo? Imewahi kunitokea. Inamfanya mtu ajisikie vyema. 1 Tim. 4:16, "*Jitunze nafsi*

yako na mafundisho. Dumu katika mambo hayo maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia."

Tunaweza kuwa baadhi ya watu walio na Biblia. Ionyeshe katika njia tunayoishi. 2 Kor. 3:2, "*Ninyi ndinyi barua yetu, iliyoandikwa mioyoni mwetu, inajulikana na kusomwa na watu wote.*"

Hitimisho

Kuna vikundi viwili vya watu wanaolidharau kanisa.

- Wale ambao si Wakristo kabisa na hawana muunganiko na kanisa. Wanalitazama kanisa kwa dharau; wanalishusha; hawalijali; hawalitilii maanani.
- Wale walioko ndani ya kanisa ambao nia zao dhidi ya kanisa si sahihi. Wanasema kwa matendo yao kwamba kanisa si muhimu kwa sababu wanalisukuma kuwa la pili katika mambo mengine ndani ya maisha yao. Wanalikataa.

Kwa nini usitowe yaliyo bora kwako, vyako vyote, kwa Kristo leo?